OFISI YA RAIS - TAMISEMI

SHULE YA SEKONDARI MIONO

SIMUNAMBA:+255787299079

Website:www.miono.ac.tz
E-Mall:info@miono.ac.tz

Kumb.Na:MSS/SR/Vol.Vll/011

SHULE YA SEKONDARI MIONO
S.L.P 26
CHALINZE
**24.03.2026**

Namba za Simu:

MkuuwaShule: +255787299079

Makamu Mkuu wa Shule: +255712665227

Matron 0766218089

Patron 0688016620

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi .............

S.L.P............................................

Yah:MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MIONO*,* **HALMASHAURI YA** CHALINZE, **MKOA** PWANI*,* **MWAKA 2026/2027**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katikaShule hii mwaka 2026/2027 na atasoma tahasusi ya .............

   Shule ya Sekondari MIONO ipo katika kijiji cha Kikaro, Kata ya **MIONO,** Tarafa ya Miono. Miono ipo jirani na MTO WAMI, ukitokea barabara kuu ya **CHALINZE-SEGERA,** shuka kituo cha **MANDERA** (baaada ya kuvuka daraja la MTO WAMI) ambapo ni njia panda ya kuelekea MIONO, utakwenda mwendo wa kilometa 20 kutokea MANDERA hadi kufika shuleni. Aidha ukitokea **SEGERA** shuka kituo cha basi cha MANDERA kabla ya WAMI. Kwa wanaotokea Dar es salaam nenda kituo cha **mabasi (daladala) cha Mbezi,** panda mabasi ya DAR-MIONO au DAR- SAADANI ambayo yanafika MIONO. Nauli ni shilingi elfu kumi na mbili (12,000/=) kutokea Mbezi, na shilingi elfu sita kutokea Chalinze. Nauli ya boda boda kutoka MIONO hadi shuleni (kitongoji cha kwa-mwala) ni shs.4,000/=
   Muhula wa masomo utaanza tarehe 06.07.2026. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 05.07.2026 akiwa na fomu zote zilizoambatanishwa katika maelekezo haya ya kujiunga.

Fomu ziwe zimejazwa kikamilifu na wahusika na kuzikabidhi shuleni wakati wa usajili.

## SARE YA SHULE

**WAVULANA**

I. Suruali 2 za heshima rangi ya dark blue zenye marinda mawili(upana wa chini usipungue inches (06) au sentimeta 15

II. Shati 2 za heshima rangi nyeupe **mikono mirefu.**

Ill. Viatu vya ngozi rangi nyeusi **SIO BUTI.** Vya kamba na visiwe na kisigino kirefu.

IV. Nguo za kushindia (shamba dress). Suruali mbili rangi ya light blue na fulana (T-shirt) mbili rangi ya dark blue (bluu iliyokolea) za kola zenye maandishi ya Miono Sekondari mgongoni na nembo ya shule kifuani**.** **(**Tshirt za dark blue zinapatikana kwenye maduka yaliyopo jirani na shule kwa gharama ya shilingi elfu kumi na tano tu zikiwa tayari zina maandishi na nembo ya Shule pia itaandikwa jina la mwanafunzi**)**

V. Soksi rangi nyeusi jozi 2.

VI. Mkanda mweusi wa kawaida usio na urembo wowote.

Vil. Tai ndefu rangi ya dark blue inayofanana na rangi ya suruali kwa wavulana.

VIII. T-shirt ya rangi ya kijivu yenye kola (grey) yenye maandishi ya Miono Sekondari mgongoni na nembo ya shule inapatikana katika maduka ya liyopo jirani na shule. Pia itaandikwa jina la mwanafunzi.

IX. Shuka mbili rangi ya bluu bahari *(lightblue)* na mto wenye foronya ya bluu bahari.

X. Sweta yenye rangi ya dark blue inayofanana na rangi ya suruali. (inapatikana katika maduka ya liyopo jirani na shule)

Xi. Track suit rangi ya kijivu**,** iwe na maandishi ya Miono sekondari mgongoni, nembo ya shule kifuani na jina la mwanafunzi la kudarizi (Track suit zinapatikana kwenye maduka yaliyopo jirani na shule)**.**

Raba na nguo za michezo jezi ya taifa stars rangi ya blue. Jezi inapatikana kwenye maduka yaliyopo jirani na shule zikiwa na maandishi ya shule mgongoni na nembo kifuani.

XI. Chandarua kwaajili ya kujikinga na mbu cha ukubwa wa 3.5 x 6 x 6

**NB: Kwa vijana wa skauti waje na sare zao za skauti**

**WASICHANA:**

III. Sketi 2 za heshima rangi ya dark blue ndefu hadi chini inayofika kwenye fundo za mguu, zenye marinda (rinda box mbele na nyuma na marinda mawili upande wa kulia na kushoto). Kitambaa kiwe kizito.

IV. Sketi moja ya heshima rangi ya bluu bahari (light blue) ndefu hadi chini kwaajili ya

Kuvaa siku ya kwenda Msikitini au Kanisani.

Ill. Shati 2 za heshirna rangi nyeupe mikono mirefu, Kwa Waislamu blauzi 2 za heshima rangi nyeupe, **mikono mirefu/ kanzufupi (shortkanzu) na hijabu ndefu inayofunika mikono.**

IV. Viatu vya ngozi rangi nyeusi **SIO BUTI.** Vyenye kamba na visiwe na kisigino kirefu,

V. Soksi ndefu rangi nyeupe.

VI. Tai ya rangi ya dark blue **(neck-tie)** inayofanana na rangi ya sketi.

VII. Kanga/kitenge doti 2

VIII. T-shirt ya rangi ya kijivu (grey) yenye maandishi ya Miono Sekondari mgongoni na nembo ya shule kifuani, pia itaandikwa jina la mwanafunzi la kudarizi inapatikana maeneo ya jirani na shule.

IX. Magauni mawili ya heshima ya kushindia (shamba dress) rangi ya pinki na light blue yawe ya marinda ya pasi, mikono mirefu **kitambaa kizito.**

X. T-shirt mbili za kushindia rangi ya dark (bluu inayofanana narangi ya suruali ya shule), **za collar** zenye maandishi ya Miono sekondari mgongoni na nembo ya shule kifuani, pia zitaandikwa jina la mwanafunzi**.** Zinapatikana kwenye maduka yaliyopo jirani na shule.

XI. Shuka mbili rangi ya pink na mto wenye foronya ya pink.

XII. Sweta_rangi ya dark blue (blue iliyokolea). Linatakiwa kua na nembo Pamoja na jina (zitapatikana shuleni)

XIII. Track suit rangi ya kijivu**,** iwe na maandishi ya Miono sekondari mgongoni, nembo ya shule kifuani na jina la mwanafunzi la kudarizi (Track suit zinapatikana kwenye maduka yaliyopo jirani na shule)**.** Raba na ]nguo za michezo jezi ya taifa stars rangi ya blue ambayo. Jezi inapatikana kwenye maduka yaliyopo jirani na shule nazo zikiwa na maandishi ya shule mgongoni na nembo kifuani.

XIV. Chandarua kwaajili ya kujikinga na mbu cha ukubwa wa 3.5x6x6.

**NB: Kwa vijana wa skauti waje na sare zao za skauti**

3. **MICHANGO MBALIMBALI**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya shule Namba 21110001592 yenye jina la MIONO SECONDARY SCHOOL FUND katika Benki ya NMB (tafadhali andika jina la Mwanafunzi kwenye pay in slip ya Benki)

**NB: Mwanafunzi aje na godoro jipya lililoshonewa kava ya plastiki. Aidha, kwa atakaekosa godoro la kunua, magodoro yanapatikana shuleni kwa kulipia shilingi elfu ishirini kwa mwaka.**

**Suruali, sketi, mashati na masweta yataandikwa majina kwa gharama ya shilingi elfu moja kila moja. Majina ni kwaajili ya kuepuka kuchanganya nguo wanafunzi hasa pindi wanapoanika nguo zao.**

Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:- Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-

(i) Madaftari aina ya "counter book quire 3" idadi 10 au zaidi
(ii) Ream mbili (02) (PAPERLINE/AONE) za karatasi size A4 (kwa mwaka)
(iii) Anashauriwa kua na vitabu vya TIE kwa masomo ya Tahasusi yake
(iv) Dissecting kit kwa mwanafunzi wa somola Biolojia na lab coat kwa wote (vinapatikana maduka ya Jirani na shule)
(v) Non-programmable Scientific calculator function 991, siyo Programmable calculator (zinapatikana maduka ya Jirani na shule)
(vi) Vyombo vya chakula (sahani,bakuli, kijiko na kikombe) **SIYO VYA PLASTIKI.**
(vii) Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko kwa matumizi binafsi ya mwanafunzi.
(viii) Mwanafunzi wa Tahasusi ya **CBG** alete fagio laini "soft broom" fagio la chelewa la wima na jembe lenye mpini.
-Wa Tahasusi ya **PCB** alete kwanja, fagio gumu "hardbroom" na fagio la chelewa la wima.
-Wa Tahasusi *ya* **PCM** alete rubber squizer, kwanja na Rake

**Vifaa hivyo vyote vianapatikana kwenye maduka ya jirani na shule kwa gharama halisi za madukani**

(i) Picha aina *ya* "passportsize" 2 za mwanafunzi na picha aina ya "pasportsize" za Wazazi/ndugu wanne wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu. Zingatia waliotajwa ndio watakao ruhusiwa kumtembelea mwanafunzi au kumwakilisha mzazi katika wito wowote shuleni.
(ii) Unaporipoti shuleni, uje na taarifa ya matokeo ya kidato cha nne **(RESULTSLIP)** halisi na nakala. Pamoja na cheti cha kuzaliwa halisi na nakala.
(iii) **Kila mwanafunzi aje na tochi kwaajili ya matumizi binafsi.**

### 4. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE BILA ONYO LA AWALI.**

1. Wizi wa aina yoyote.
2. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro (Iii)Kutoingia darasani hata kama yupo shuleni.
3. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
4. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
5. Kugoma na kuhamasisha mgomo
6. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla
7. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyete yule.
8. Hairuhusiwi kufuga ndevu, Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
9. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya.
10. Uvutaji wa sigara.
11. Uasherati, uzinzi, uhusiano wa ki-mapenzi, kuoa au kuolewa
12. Kupata ujauzito au kutoa mimba
13. Kudharau wimbo na bendera yaTaifa
14. Kumiliki, kutumia au kukutwa na simu ya mkononi katika mazingira ya shule
15. Hairuhusiwi kulala nje ya shule bila ruhusa/kibali cha Mkuu wa Shule
16. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
17. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi
18. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.

MUHIMU:

1. **Mwanafunzi hapaswi kuja na *simu* shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeru usiwa kutunza simu ya mwanafunzi**

2. **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

3. **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**
4. ***MWANAFUNZI ANAPORUDI SHULENI KUTOKA LIKIZO NI LAZIMA AFIKE SHULENI SIKU/TAREHE YA-KUFUNGUA SHULE, KINYUME CHA HAPO MZAZI ATALAZIMIKA KUMLETA SHULENI, MWANAFUNZI PEKE YAKE HATAPOKELEWA***

*Mzazi/Mlezi unashauriwa kumfungulia mwanao akaunti ya benki kwaajili ya kumtumia fedha* za *matumizi,*
***MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUMILIKI LAINI YA SIMU KATIKA MAZINGIRA YA SHULE***

**UTHIBITISHO WA KUKUBALI NA FASI YAKUINGIA KIDATO CHA TANO SHULEYA SEKONDARI MIONO**

**SEHEMUA (ijazwe na mwanafunzi)**

Mimi (jina kamiLI)..........................................................................................................................................

Nilizaliwa tarehe.........................mwezi.......................mwaka...........................................

Mahali nilipozaliwa kijiji/Mtaa...........................................Wilaya.....................................

Mkoa..............................................................Dini.......................................................

Nakubali nafasi niliyopewa ya kuingia kidato cha TANO shule ya sekondari MIONO. Nathibitisha kuwa nitatii na kuzifuata sheria na kanuni za shule ambazo mwanafunzi analazimika kutekeleza nakutimiza. Najua nakuamini kwamba migomo na vurugu siyo njia sahihiya kutatua matatizo katika jamii, hivyo naahidi kutoshiriki katika migomo wala vurugu zozote bali nitakuwa mstari wa mbele kutoa taarifa kwa uongozi wa shule ili uweze kutatua au kutafutia utatuzi wa changamoto zozote zitakazojitokeza shuleni.

Saini......................................................................tarehe...................................................

**SEHEMUB (ljazwenamzazi/mlezi)**

Mimi(jinakamili)...........................................................................................................
Wa Kijiji cha/mtaa wa............................................. Wilaya ya Mkoa wa …………......................

Kazi yangu ni.............................................................. *Dini* ...........................................

Nambari ya simu.........................................................................

Nafurahi kupokea nafasi aliyopata mtoto wangu, nitatekeleza na kutimiza mahitaji yote ya mtoto wangu kulingana na maagizo ya shule. Pia nitahakikisha mtoto anaenda shule kwa muda uliopangwa na nitakuwa tayari wakati wowote kusaidiana na shule kumlea mtoto huyu kinidhamu na kimaadili.
Saini ya mzazi/mlezi...............................
Jina la mtendaji wa kijiji/Kata..........................................................................Saini........................

Mwisho, Karibu sana Shule ya Sekondari MIONO ili ufaidike kwa kupata ELIMU BORA.

…………………..

**EXAUD R. MTEWELE**

**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE MIONO SEKONDARI
S. L. P. 26
CHALINZE
PWANI

**FORMB (PARTA)**

**PRESIDENTS'OFFICE**

**LOCAL GOVERNMENT AND REGIONAL ADMINISTRATION**

***TEL:+255787299079,***
***+255712665227***

**MIONO SECONDARY CHOOL**
**P.O.BOX 26**
**CHALINZE**
**TAREHE..................**

**REF.NO:MSS/F.V.SEU2024/24/002 TO:**

**THE MEDICAL OFFICER,**

**RE:REQUEST FORMEDICAL EXAMINATION TO:**
**Mr./MISS.......................................................................................................FORM 5 - 2026/2027**

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time Schooling course. The Examination should include the following categories [i-iii].

Each category or sub-category of which will render the applicant ineligible incase of a Defect. Pregnancy (category IV) will also render a girl candidate ineligible to the course.

(i) (a)Eye________________________________________

(b) Hearing______________________________________

(c) Limbs_______________________________________

(d) Speech______________________________________

(e) Venereal disease (s)________________________________

(f) Leprosy______________________________________

(g) Epilepsy______________________________________

(ii) Neuroses______________________________________
(iii) Other serious diseases________________________________
(iv) Pregnancy_______________________________________

.......................

**EXAUD R. MTEWELE**

**HEADMASTER**

...........................

Name, signature and official stamp

**OFFICER IN CHARGE**

MKUU WA SHULE MIONO SEKONDARI
S. L. P. 26
CHALINZE
PWANI